

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI



MAMLAKA YA UDHIBITI WA  
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI  
(EWURA)



***KUMB: PPR/2021 - 02/1***

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI  
KUANZIA JUMATANO, TAREHE 3 FEBRUARI 2021**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 3 Februari 2021**. Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za rejareja na jumla za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyopokelewa kupitia **Bandari ya Dar es Salaam** zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 6 Januari 2021. Kwa Februari 2021, bei ya rejareja ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa shilingi 53/Lita (sawa na asilimia 2.89), shilingi 134/Lita (sawa na asilimia 7.89) na shilingi 119 (sawa na asilimia 7.19), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei ya jumla ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa shilingi 52.90/Lita (sawa na asilimia 3.10), shilingi 133.36 (sawa na asilimia 8.51) na Shilingi 118.31/lita (sawa na asilimia 7.77), mtawalia.
- (b) Kwa Februari 2021, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimebadilika ikilinganishwa na bei zilizotolewa tarehe 6 Januari 2021. Kwa mwezi Februari 2021, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 91/lita (sawa na asilimia 4.99) na shilingi 80/lita (sawa na asilimia 4.54), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 90.92/lita (sawa na asilimia 5.35) na shilingi 79.48/lita (sawa na asilimia 4.89) mtawalia. Hata hivyo, bei za Mafuta ya Taa hazina mabadiliko na zitaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo la tarehe 6 Januari 2021. Hii ni kwa sababu, kwa Januari 2021 hakuna shehena ya Mafuta ya Taa iliyopokelewa kupitia bandari ya Tanga.
- (c) Kwa Februari 2021, bei za rejareja na jumla kwa bidhaa za mafuta ya Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kusini (Mtwara, Lindi, and Ruvuma)**

zimebadilika ikilinganishwa na bei zilizotolewa tarehe 6 Januari 2021. Kwa Februari 2021, bei ya rejareja ya Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 71/lita (sawa na asilimia 3.89) na Shilingi 76/lita (sawa na asilimia 4.34). Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei ya jumla ya Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 70.98/lita (sawa na asilimia 4.16) na Shilingi 75.87/lita (sawa na asilimia 4.67).

- (d) Mabadiliko haya ya bei yanachangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (*BPS Premium*).
- (e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (f) Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166**, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (g) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu **bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 656 la tarehe 21 Agosti 2020.**
- (h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei

kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

### JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	<b>1,887</b>	<b>1,829</b>	<b>1,769</b>
<b>Arusha</b>	<b>1,976</b>	<b>1,890</b>	<b>2,051</b>
Arumeru (Usa River)	1,976	1,890	2,051
Karatu	1,994	1,909	2,069
Longido	1,987	1,901	2,062
Monduli	1,981	1,896	2,056
Monduli-Makuyuni	1,986	1,900	2,061
Ngorongoro (Loliondo)	2,061	1,975	2,136
<b>Pwani (Kibaha)</b>	<b>1,891</b>	<b>1,834</b>	<b>1,773</b>
Bagamoyo	1,898	1,840	1,780
Bagamoyo (Miono)	1,928	1,871	1,811
Chalinze Junction	1,901	1,843	1,783
Chalinze (Msata)	1,905	1,848	1,787
Kibiti	1,907	1,850	1,789
Kisarawe	1,894	1,836	1,776
Mkuranga	1,896	1,839	1,779
Rufiji	1,914	1,857	1,797
<b>Dodoma</b>	<b>1,945</b>	<b>1,888</b>	<b>1,828</b>
Bahi	1,953	1,895	1,835
Chamwino	1,941	1,883	1,823
Chemba	1,972	1,914	1,854
Kondoa	1,978	1,921	1,860
Kongwa	1,943	1,885	1,825
Mpwapwa	1,947	1,889	1,829
Mtera (Makatopora)	1,964	1,907	1,847
Mvumi	1,952	1,894	1,834
<b>Geita</b>	<b>2,052</b>	<b>1,995</b>	<b>1,934</b>
Bukombe	2,041	1,984	1,923
Chato	2,073	2,016	1,955
Mbogwe	2,090	2,033	1,972
Nyang'hwale	2,067	2,010	1,949
<b>Iringa</b>	<b>1,951</b>	<b>1,893</b>	<b>1,833</b>
Ismani	1,956	1,898	1,838
Kilolo	1,955	1,898	1,837
Mufindi (Mafinga)	1,961	1,903	1,843
Mufindi (Igowole)	1,969	1,912	1,852
<b>Kagera (Bukoba)</b>	<b>2,102</b>	<b>2,045</b>	<b>1,984</b>
Biharamulo	2,077	2,019	1,959

Karagwe (Kayanga)	2,119	2,061	2,001
Kyerwa (Ruberwa)	2,124	2,067	2,007
Muleba	2,102	2,045	1,984
Ngara	2,090	2,033	1,972
Misenyi	2,111	2,053	1,993
<b>Katavi (Mpanda)</b>	<b>2,095</b>	<b>2,037</b>	<b>1,977</b>
Mlele (Inyonga)	2,114	2,056	1,996
Mpimbwe (Majimoto)	2,088	2,030	1,970
Tanganyika (Ikola)	2,113	2,055	1,995
<b>Kigoma</b>	<b>2,118</b>	<b>2,061</b>	<b>2,000</b>
Uvinza (Lugufu)	2,130	2,073	2,013
Buhigwe	2,107	2,050	1,990
Kakonko	2,075	2,018	1,957
Kasulu	2,104	2,047	1,986
Kibondo	2,082	2,025	1,965
<b>Kilimanjaro (Moshi)</b>	<b>1,966</b>	<b>1,880</b>	<b>2,041</b>
Hai (Bomang'ombe)	1,969	1,883	2,044
Mwanga	1,959	1,873	2,034
Rombo (Mkuu)	1,982	1,897	2,057
Same	1,952	1,866	2,027
Siha (Sanya Juu)	1,972	1,887	2,047
<b>Lindi</b>	<b>1,917</b>	<b>1,842</b>	<b>1,828</b>
Lindi-Mtama	1,922	1,847	1,846
Kilwa Masoko	1,941	1,866	1,803
Liwale	1,953	1,878	1,849
Nachingwea	1,937	1,862	1,857
Ruangwa	1,943	1,869	1,859
<b>Manyara (Babati)</b>	<b>2,010</b>	<b>1,924</b>	<b>2,085</b>
Hanang (Katesh)	2,021	1,935	2,095
Kiteto (Kibaya)	2,025	1,940	2,100
Mbulu	2,023	1,937	2,098
Simanjiro (Orkasumet)	2,042	1,956	2,117
<b>Mara (Musoma)</b>	<b>2,065</b>	<b>2,008</b>	<b>1,948</b>
Musoma Vijijini (Busekela)	2,106	2,049	1,988
Rorya (Ingirijuu)	2,074	2,017	1,956
Rorya (Shirati)	2,109	2,051	1,991
Bunda	2,056	1,999	1,939
Bunda (Kisorya)	2,066	2,009	1,948
Butiama	2,062	2,005	1,944
Serengeti (Mugumu)	2,111	2,053	1,993
Tarime	2,076	2,019	1,959
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,081	2,023	1,963
<b>Mbeya</b>	<b>1,994</b>	<b>1,936</b>	<b>1,876</b>
Chunya	2,003	1,946	1,886
Chunya (Makongolosi)	2,018	1,960	1,900
Kyela	2,010	1,952	1,892
Mbarali (Rujewa)	1,978	1,920	1,860
Rungwe (Tukuyu)	2,003	1,945	1,885
<b>Morogoro</b>	<b>1,912</b>	<b>1,854</b>	<b>1,794</b>
Mikumi	1,927	1,870	1,810

Kilombero (Ifakara)	1,950	1,892	1,832
Kilombero (Mlimba)	1,972	1,914	1,854
Kilombero (Mngeta)	1,961	1,904	1,843
Ulanga (Mahenge)	1,960	1,903	1,842
Malinyi	1,970	1,913	1,853
Kilosa	1,930	1,873	1,812
Gairo	1,930	1,873	1,812
Mvomero (Wami Sokoine)	1,922	1,865	1,804
Mvomero (Sanga Sanga)	1,912	1,854	1,794
Turiani	1,937	1,879	1,819
<b>Mtwara</b>	<b>1,903</b>	<b>1,829</b>	<b>1,841</b>
Nanyumbu (Mangaka)	1,940	1,865	1,890
Masasi	1,920	1,845	1,867
Newala	1,924	1,850	1,873
Tandahimba	1,917	1,843	1,867
Nanyamba	1,917	1,843	1,867
<b>Mwanza</b>	<b>2,037</b>	<b>1,979</b>	<b>1,919</b>
Kwimba	2,055	1,997	1,937
Magu	2,045	1,987	1,927
Misungwi	2,031	1,974	1,913
Sengerema	2,069	2,012	1,952
Ukerewe	2,096	2,039	1,979
<b>Njombe</b>	<b>1,979</b>	<b>1,922</b>	<b>1,861</b>
Njombe (Kidegembye)	2,000	1,942	1,882
Ludewa	2,017	1,960	1,899
Makambako	1,971	1,914	1,854
Makete	2,010	1,952	1,892
Wanging'ombe (Igwachanya)	1,977	1,919	1,859
<b>Rukwa (Sumbawanga)</b>	<b>2,060</b>	<b>2,002</b>	<b>1,942</b>
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,060	2,002	1,942
Kalambo (Matai)	2,067	2,009	1,949
Nkasi (Namanyeje)	2,073	2,016	1,955
<b>Ruvuma (Songea)</b>	<b>1,989</b>	<b>1,914</b>	<b>1,892</b>
Mbinga	2,002	1,927	1,926
Namtumbo	1,980	1,905	1,922
Nyasa (Mbamba Bay)	2,027	1,952	1,936
Tunduru	1,954	1,880	1,951
<b>Shinyanga</b>	<b>2,016</b>	<b>1,958</b>	<b>1,898</b>
Kahama	2,029	1,972	1,912
Kishapu	2,044	1,987	1,926
Ushetu (Nyamilangano)	2,047	1,989	1,929
Salawe	2,030	1,973	1,913
<b>Simiyu (Bariadi)</b>	<b>2,057</b>	<b>2,000</b>	<b>1,939</b>
Busega (Nyashimo)	2,050	1,993	1,932
Itilima (Lagangabilili)	2,060	2,003	1,942
Maswa	2,049	1,991	1,931
Meatu (Mwanhuzi)	2,056	1,998	1,938
<b>Singida</b>	<b>1,977</b>	<b>1,920</b>	<b>1,860</b>
Iramba	1,990	1,932	1,872
Manyoni	1,962	1,905	1,844

Itigi (Mitundu)	1,978	1,920	1,860
Ikungi	1,973	1,915	1,855
Mkalama (Nduguti)	2,002	1,944	1,884
<b>Songwe (Vwawa)</b>	<b>2,003</b>	<b>1,946</b>	<b>1,885</b>
Songwe (Mkwajuni)	2,010	1,952	1,892
Ileje	2,007	1,949	1,889
Momba (Chitete)	2,012	1,955	1,894
Tunduma	2,007	1,950	1,889
<b>Tabora</b>	<b>2,041</b>	<b>1,983</b>	<b>1,923</b>
Igunga	1,995	1,937	1,877
Kaliua	2,060	2,002	1,942
Ulyankulu	2,054	1,997	1,936
Nzega	2,005	1,948	1,888
Sikonge	2,053	1,995	1,935
Urambo	2,054	1,997	1,936
Uyui	2,042	1,984	1,924
<b>Tanga</b>	<b>1,919</b>	<b>1,834</b>	<b>1,994</b>
Handeni	1,940	1,854	2,015
Kilindi	1,955	1,869	2,030
Korogwe	1,932	1,846	2,006
Lushoto	1,941	1,855	2,016
Mkinga (Maramba)	1,926	1,841	2,001
Muheza	1,924	1,839	1,999
Pangani	1,926	1,840	2,001

#### JEDWALI B: BEI ZA JUMLA

	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
DAR ES SALAAM	1,758.70	1,700.97	1,641.54
TANGA	1,791.33	1,705.54	1,866.20
MTWARA	1,775.33	1,700.66	-

**Inj. Godfrey H. Chibulunje**  
**MKURUGENZI MKUU**  
**EWURA**